JIJI LA GRAND RAPIDS

# SERA YA UTAWALA

| | |
|---|---|
| **NAMBARI: 17-02** | **TAREHE: 1 Oktoba, 2017** |
| **SASISHO:** | |
| **IMETOLEWA NA: Meya wa Jiji** | **IMESAINIWA:** |

**MAUDHUI**: **KITENDO CHA KUJIELEZA KATIKA ENEO LA UMMA**

**DHUMUNI:** Sera hii imedhumunia kutoa mwongozo kwa wafanyakazi wa Jiji, wa ushughulikiaji wa shughuli zinazohusisha vitendo vya uhuru wa kujieleza ulindwao na Marekebisho ya Kwanza katika Katiba ya Marekani.

**UTANGULIZI:**

## I. KAULI YA SERA

Meya wa Jiji ameweka sera ifuatayo ili kuhimiza uhuru wa mabadilishano ya hoja na usemi ulindwao na Katiba ya Marekani, katika eneo la umma, huku ikitoa muongozo kwa wananchi na wafanyakazi wa Jiji uhusianao na taratibu na kanuni zipelekeazo matumizi ya amani na ya kistaarabu ya maeneo ya umma. Sera hii itatumika katika kitendo kilichofanywa ndani ya maeneo ya umma, majengo yote, hifadhi, ama mahala pengine panapomilikiwa au kusimamiwa na Jiji la Grand Rapids. Miongozo inayofuata Sera hii itatangazwa na Meya wa Jiji ili kuisaidia umma katika kupanga na kutekeleza shughuli za aina hiyo.

A. Fafanuzi.

"*Kitendo cha Kujieleza*" kwa madhumuni ya sera hii humaanisha tendo lolote la usemi ama onyesho lilindwalo na Marekebisho ya Kwanza ya Katiba ya Marekani, hili ni pamoja na mkusanyiko wowote wa mtu mmoja au zaidi katika eneo la umma kwa makusudi ya kushiriki katika kitendo hicho, ni pamoja na, ila si tu:

1. Vikao na shughuli nyingine za makundi;
2. Hotuba, maonyesho, maandamano, maadhimisho, mikesha na matukio mengineyo; na
3. Usambazaji wa fasihi, kama vile vipeperushi na vijitabu.



B. Kitendo cha Kujieleza si sawa na "Tukio Maalum". Waratibu wa Vitendo vya Kujieleza wanaweza kwa hiari kuamua kukata Kibali cha Tukio Maalum, ikiwa watachagua kufanya hivyo. Kwa matukio yafanyikayo kwa kufuata Kibali cha Tukio Maalum, matakwa ya Sura ya 53 "Matukio Maalum" yatazingatiwa.

C. Mauzo ya bidhaa, chakula au huduma si "Kitendo cha Kujieleza". Shughuli kama hiyo ya biashara si kitendo cha kujieleza kinacholindwa chini ya Katiba, na hivyo kinapaswa kufuata mchakato wa kibali cha Tukio Maalum.

D. Sera hii haipaswi kufasiriwa kuwa kama kizuizi cha Kitendo cha Kujieleza kilindwacho chini ya Marekebisho ya Kwanza ya Katiba ya Marekani, nje ya muda stahiki, eneo na namna zilizoelezewa humu ndani.

## II. <u>TARATIBU NA MIONGOZO</u>

A. **Notisi Haihitajiki.** Notisi ya awali kwenda kwa Jiji haihitajiki. Hata hivyo, ili kuweza kupangilia kwa ubora zaidi rasilimali za Jiji, na kuhakikisha usalama wa raia, waratibu wanahimizwa kutoa taarifa kadri iwezekanavyo katika ofisi za Jiji litakalobeba kitendo kilichoratibiwa.

B. **Uratibu Kiujumla.** Wafanyakazi wa Jiji wanaweza kufahamu juu ya shughuli zilizopangwa na wanaweza kuwasiliana na mratibu (waratibu) husika na kutoa usaidizi wao ili kupunguza changamoto za kiratibu zinazoweza kujitokeza kama vile watu wengi kuhifadhi eneo moja ama kuhifadhi eneo lisilofaa, masuala ya ujenzi ama mifungamano wa watu, au changamoto nyingine za kiratibu.

C. **Makadirio ya Umati**. Ili kutazamia idadi ya washiriki wanaotarajiwa kushiriki shughuli ya madhumuni ya sera hii, maafisa wa Jiji wanaweza kutumia taarifa yoyote au chanzo cha taarifa kinachoweza kutumiwa na mtu katika kutambua mipango ya shughuli, inayojumuisha, ila si tu, taarifa zilizopatikana kutoka kwa mratibu (waratibu) wa tendo husika, matangazo katika redio, chapisho, runinga, intaneti ama mtandao wa kijamii; na wafanyakazi wa Jiji

watalinganisha tukio hilo na watu waliojitokeza katika matukio yaliyopita yanayofanana na hayo.

D. **Maandamano na Upingaji Maandamano**. Ikiwa waratibu wa Kitendo cha Kujieleza kinachoangazia malengo, sababu, vitendo ama sera zinazopingana, watataka kutumia barabara, hifadhi ama jengo lile lile kwa wakati mmoja, Jiji linaweza kupanga sehemu ndani ya eneo hilo katika msingi wa usawa, sawasawa na idadi ya malengo yanayoadhirishwa. Wakati wa kugawa maeneo kama ilivyoelezewa katika aya hii, Jiji kwa kadri itakavyoweza kufanya na kwa kadri ya usalama, itaweka jitihada stahiki kuwaweka washiriki wote katika nafasi itakayowawezesha kuonekana na kusikika na hadhara yao waliyoikusudia.



E. **Maeneo yaliyohifadhiwa kupita kiasi ama yasiyofaa**. Endapo kama hali yoyote katika zifuatazo itajitokeza, Meya wa Jiji ama mwakilishi wake atapaswa kufanya juhudi kuwasiliana na mratibu ili kumjulisha kwamba shughuli iliyopangwa:

1. Inatarajiwa kusababisha ama kupelekea umati mkubwa kuliko umati unaowezwa kubebwa kwa usalama ndani ya eneo husika; ama

2. Ina uwezekano wa kukiuka Kanuni za Hifadhi; ama

3. Ina uwezekano wa kuvuruga ama kuingilia mradi wa ujenzi, tukio lenye kibali, hifadhi ya maegesho, ama programu za Jiji; au

4. Ina uwezekano wa kuingilia uingizi au utokaji wa watu au magari katika hospitali, kituo cha uzimaji moto, ama jengo lingine la ushughulikiaji dharura; ama

5. Ina uwezekano wa kuzuia ufikivu wa makutano yoyote ya njia kuu, ikiwa ni pamoja na miteremko, barabara na madaraja; ama

6. Si Kitendo cha Kujieleza, bali badala yake ni Tukio Maalum linalohitaji kibali chini ya Kifungu B cha Sera hii, ama matakwa yoyote ya Sura ya 53 ya Sheria za Jiji (“Matukio Maalum”).

Wafanyakazi wa Jiji kwa nia njema watafanya jitihada kushirikiana na mratibu husika ili kutatua changamoto kama hizo kupitia, kwa mfano, kutafuta mpangilio stahiki mbadala ama mazingira yatakayotatua uwezo, hitilafu ama masuala mengine ya kiratibu.

F. **Utangazaji wa Miongozo na Vigezo vya Mwenendo**

Meya wa Jiji ama mwakilishi wake ana mamlaka ya kutangaza Miongozo na Vigezo vya Mwenendo vilivyopo kulingana na Sera hii. Miongozo na Vigezo hivyo vya Mwenendo vitachapishwa na kutolewa kwa umma kupitia tovuti ya Jiji.

G. **Ada na Tozo**

Jiji halitatoza ada, ama kuhitaji bima, ama fidia, kuwa kama malipo ya kufanya kitendo cha kujieleza sawasawa na kilivyofafanuliwa humu ndani.



H. **Usitishaji wa Dharura na Malipo kwa Halaiki**

Kitendo cha Kujieleza kinaweza kusitishwa kutokana na uwepo wa madhara ya kiusalama, afya na ustawi wa umma kwa msingi wa uwepo wa hatari za kiulinzi, kiusalama, ama hali ya hewa. Wawakilishi wa wafanyakazi wa Jiji waliotajwa hapa chini watawajibika kufanya maamuzi ya usitishaji, na kuwasilisha maamuzi hayo kwa waratibu, kwa hatari zote zilizoainishwa, na kwa wakati huo wanaweza kusimamia usambaratishaji wa watu waliokusanyika na kuchukua hatua ya kisheria stahiki kutekeleza oda hiyo:

1. Afisa Komando wa Polisi awapo eneo la tukio: anaweza kusitisha tukio kwa sababu za hali ya hewa, za kiusalama, ama hatari za ulinzi, baada ya jitihada zote kufanyika kutatua masuala ya kiusalama au ulinzi.

2. Kiongozi wa Kikosi cha Uzima Moto ama mwakilishi wake: anaweza kusitisha tukio kutokana na hatari za moto ama zinazohusiana na moto au nyenzo hatarishi.

3. Wafanyakazi Viongozi wa Hifadhi na Vitengo vya Burudani: wanaweza kusitisha tukio kutokana na hatari za hali ya hewa pindi tukio linapofanyika eneo la hifadhi.

**KIAMBATISHI: Miongozo na Vigezo vya Mwenendo**